

HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI


(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W) Mbarali)

MKOA WA MBEYA

Simu ya Mezani: 252957440/252957447

Barua Pepe: ded@mbaralidc.go.tz

Tovuti: www.mbaralidc.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)

S.L.P 237,

RUJEW A

Unapojibu tafadhali taja

Kumb. Na. MDC/S.20/VOL.V/5/166

07/05/2020

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa watazania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi za kazi kama ifuatavyo:-

MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA III – NAFASI 3

Sifa za Mwombaji:-

1. Awe na Elimu ya Kidato cha Nne/Sita
2. Awe na Cheti/Astahada NTA Leve 5 katika moja ya fani zifuatazo:
 - Utawala
 - Rasilimali watu
 - Sheria
 - Maendeleo ya Jamii
 - Elimu ya Jamii
 - Usimamizi wa Fedha au
 - Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

MSHAHARA

Mshahara utanzia Ngazi ya TGS B

MAJUKUMU YA KAZI

- Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji
- Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji
- Kuratibu Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na taratibu za uendeshaji wa Serikali ya Kijiji
- Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umasikini na kuongeza uzalishaji mali
- Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za Kijiji

MASHARTI YA JUMLA

- Awe Raia wa Tanzania
- Awe na Umri wa Miaka 18 hadi 45
- "Testimonials, Provisional Results, Statement of Result" na hati za matokeo kidato cha Nne na Sita (form IV na VI Result Slips) **HAVITAKUBALIWA.**
- Waombaji waliosoma Nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimekaguliwa na kuthibitishwa na mamlaka husika (NECTA, NACTE na TCU)
- Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwa kuomba isipokuwa kama wana Kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- Uwasilishaji na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua Stahiki za Kisheria
- Waombaji wote kwenye barua zao za maombi waandike namba za simu za uhakika kwa ajili ya mawasiliano

NAMNA YA KUTUMA MAOMBI;-


Kila muombaji wa kazi awasilishe barua iliyoandikwa kwa mkono ikiambatana na;-

- Wasifu Binafsi (CV)
- Vivuli vya Vyeti vya Elimu na Ujuzi
- Majina matatu ya wadhamini
- Cheti cha kuzaliwa
- Picha mbili za "Passport Size"

Maombi yote yatumwe kupitia anuani ya posta kama ifuatavyo:-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya,
S.L.P 237,
RUJEWANA – MBARALI.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 28/05/2020 Siku ya Alhamisi, muda wa 9.30 alasiri


Kivuma H. Msangi,
MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA,
MBARALI.

